# KANISA LINAPASWA KUJIWEKA TAYARI ILI LISIJE LIKABAKI DUNIANI SIKU YA UNYAKUO

# MAANDIKO: MATH. 24: 36 – 44, 1KOR. 15: 49 – 52, 1THES. 4: 13 – 17.

1. **UTANGULIZI:**

   Pamoja na ahadi nyingi ambazo Mungu amelipa Kanisa, yaani **baraka za kiroho na kimwili**- kulindwa, kuponywa, kuinuliwa kiuchumi, ushindi katika vita na majaribu, kipawa cha Roho Mtakatifu kama mwalimu na kiongozi katika safari yetu n.k. iko ahadi moja kubwa ya thamani sana ambayo nataka leo tujikumbushe.

   **Yoh. 14: 1 – 3 – Ahadi ya kuandaliwa makao mazuri ambayo tutakwenda kukaa na Bwana milele na milele**; **1Thes. 4: 17.**

- Ni fahari na heshima iliyoje kuandaliwa na Yesu makao Mbinguni ***ufun. 21, Ebr. 13: 14***
- Wakati Yesu anawaambia wanafunzi wake kuwa ataondoka, walijaa fadhaa nyingi walitamani kuendelea kukaa naye duniani lakini baada ya kuwaeleza lengo la yeye kwenda ni ili kuandaa makao mazuri kwa ajili yao walifarijika, wakafurahi, wakajaa matumaini makubwa.
- Unajua sisi wana wa Mungu tunaweza kukaa hapa duniani tukifurahia fahari zake na wakati mwingine tukamsahau hata Mungu kwa sababu hatujapata ufunuo halisi wa yale mema aliyotuandalia Mungu baada ya maisha haya. Nataka nikutie moyo mtu wa Mungu, hata kama unapitia katika changamoto mbalimbali usikate tamaa, usife moyo - yako mema ambayo Mungu ametuandalia na **mambo hayo yatarithiwa na watu waaminifu katika Kristo Yesu, walioendelea kuishindania imani mpaka mwisho kwa kuishinda dhambi, dunia na shetani. Math. 7:21, Ufun. 21:7**

- **Maandiko hapo juu yanaonyesha kuwa Kristo atarudi tena duniani, kurudi huku kutakuwa kwa awamu mbili:-**

1. **Kurudi kuja kulichukua Kanisa - Unyakuo. 1Thes. 4: 16 – 17.**

- **Kunyakua –** Ni **kupora kitu, kubeba kwa haraka, ghafla kama vile mwewe anavyomnyakua kuku – Ni tukio la kushtukiza.**

- Wakati huu Yesu atakaa juu mawinguni kati ya mbingu na dunia, wafu waliokufa katika Bwana (Watakatifu) watafufuliwa kwanza kisha

watakatifu walio hai watabadilishwa ili wavae mwili wa Mbinguni usio na uharibifu**. 1Kor. 15: 50 – 54, Filp. 3: 20 – 21**- Kisha wote kwa pamoja watanyakuliwa kumlaki Bwana wao hewani.

- Tukio hili ni siri ya Mungu, hata Yesu hajui ni lini atarudi**. Math. 24: 36.**

2. **<u>Kurudi baada ya dhiki kuu kwa hukumu na kuanzisha utawala wake duniani. Math. 25: 31 – 46, Ufun. 20</u>**

- Wakati Kristo akiwa kwenye karamu na washindi huko juu. Hapa duniani kutakuwa na dhiki kuu mfano wake haujawahi tokea. ***Math. 24: 21***, ***Ufun. 6 – 18 –*** Dhiki hii itawapata wale walioshindwa kumwamini Yesu kama Bwana na Mwokozi wao. Wengine wataokoka katika dhini Kuu kwa mateso makali. Baada ya dhiki kuu ndipo Kristo atarudi tena katika utukufu na nguvu kama hakimu. Tukio hili siyo la ghafla litatanguliwa na ishara na ajabu nyingi

- Tunaona kuwa mada kuu ni Kanisa kujiweka tayari, tutaona maana ya kujiweka tayari na ni kwanini tujiweke tayari?

1. **<u>KUJIWEKA TAYARI. Math. 24: 44</u>**

i. **<u>Ni kukesha -Keep watch – gregoreo (Gk)-</u> kudumu katika kuwa macho kiroho. Math 25:13, Math. 13:24-28a(25)** watu walipolala adui akapanda magugu. Usingizi wa kiroho unaleta madhara- **kudumu katika kuomba, soma neno upate ufahamu. Math 22:29, Kol. 4:2.**
   - **1Yoh. 4:1.** Biblia inatuagiza kuzijaribu roho maana waharibifu ni wengi wanaotafuta kuighoshilmani yetu. **Math 24:4-5,11**

ii. **Ni kujilinda, kuwa makini, kuishi kwa tahadhari katika dunia. 1Yoh. 2:15-17.** Dunia siyo rafiki imejaa uovu wa kila aina, ukiwa mtu wa kwenda mbio nayo, utampoteza Yesu njiani. **Yak 4:4, Rum 12:2, 1Yoh. 5:18**

iii. **<u>Ni kudumu na kusimama Imara katika Imani bila kuyumba mpaka mwisho. Kol. 1:23, Yak 5:8</u>**
   - **Luk 18:8** Yesu aliuliza swali "**walakini, atakapokuja mwana wa Adamu, je ataiona Imani duniani"**Yesu alikuwa na mashaka kutokana na dhiki, majaribu na adha zilizo duniani na madanganyo mengi je watu watadumu katika Imani? Mungu bado anatamaani kuona watu wenye uwezo wa **kulinda na kuitetea Imani katikati ya kizazi kilichoharibika.** Kama Nuhu aliweza kusimama peke yake, Mikaya, Paulo. **2Tim. 4:7-8** – sisi tuna shida gani?
   - Tunapaswa kuuonyesha ulimwengu Imani/ wokovu wa kweli

## 2. NI KWANINI TUJIWEKE TAYARI?

i. **Hatujui siku wala saa atakayokuja Bwana** itakuwa ni ghafla, hivyo basi maandalizi yanahitajika sasa. **Math 24:44;**

- **Math 25:1-13** Wanawali hawa wote walilala lakini tunaona wenye busara walikuwa wamejiandaa taa zai zilijaa mafuta
- Wapumbavu walikuwa na taa bila mafuta ya kutosha
  **Taa- Zab. 119:105-** Ni neno la Mungu
  **Mafuta – 1Yoh 2:27**- Ni Roho Mtakatifu
- Tukipunguza vitu vya Mungu kwa ajili ya masumbufu ya maisha siku ile tutakwama mlangani- lazima tujae nguvu za Roho Mtakatifu na neno la Mungu liwe dira yetu, Roho Mtakatifu atachukua udhaifu wetu, atatusaidia kuomba ipasavyo, atatutia nguvu. **Rum 8:26-27, Mdo 1:8. Galt. 5: 16-18**

ii. **Jiji tunalokwenda kuishi linaingia watu makini waliojiandaa-Ufun. 21:27**

- Watu waaminifu walioikinai dunia na mambo yake, waliokuwa tayari kuongozwa na Roho wa Mungu hao ndio watakaopenya pale.
  **Rum 8:8-14**

iii. **Safari ya Mbinguni ina vita vikali sana inahitaji kujikana- Luk 13:24**

- **"Biblia inasema wengi watataka kuingia wasiweze"**, waitwao ni wengi lakini wateule ni wachache. **Math 22:14**
- Hivyo basi ni lazima mtu awe tayari kuachilia matakwa yake ili afanye mapenzi ya Mungu
- **Mith 4:23**- lazima awe tayari kulinda moyo wake ili uwe stoo ya mema wala si mabaya. Awe tayari kuutoa mwili wake uwe dhabihu kwa Mungu- **Rum 12:1**

**Mambo ya kufanya**

- Jikague kiroho chako mara kwa mara ulivyoanza na ulivyo sasa. **2Kor 13:5**
- Rekebisha mapungufu yako mara moja
- Kubali kukosolewa/ kurekebishwa na Neno La Mungu- mahubiri/ mafundisho, wapendwa wenzako, watumishi wa Mungu n.k
- Jibidishe katika kuabudu, kuomba, kusoma neno la Mungu na kumtumikia Mungu
- Jiombee kila siku kuwa na mwisho mwema. **Mhub 7:8a, Ezek. 18:24**

***Mbarikiwe na Bwana***
***Dr. A.L. Mwizarubi (Mrs)***
***30/1/2022***